

Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Venance Mabeyo akiwahutubia wananchi wakati wa shughuli ya mazishi ya kitaifa iliyofanyika uwanja wa Magufuli, Chato mkoani Geita juzi. (Na Mpigapicha Maalumu).

* HABARI LEO UK 8. Ukuzaji viumbe maji kuanzishwa halmashauri 80 *

Na John Nditi, Morogoro

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22 ina mpango wa kuanzisha vituo vya ukuzaji viumbe maji katika halmashauri za wilaya 80 vitakavyotumika kama shamba darasa kufundishia wananchi ufugaji samaki.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema hayo mjini Morogoro mbele ya Kamati

ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji ilipotembelea kituo cha ukuzaji viumbe maji kinachozalisha vifaranga vya samaki cha Kingolwira, Manispaa ya Morogoro.

Alisema lengo ni kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na kituo hicho ambacho kitatumika kama shamba darasa kwa ajili ya kufundisha wananchi namna ya kufuga samaki.

Waziri Ndaki alisema mkakati wa serikali kupitia vituo hivyo

vitakavyokuwepo katika halmashauri zote za wilaya ni kuwa na samaki wengi wafugwao kwa njia mbalimbali yakiwemo mabwawa na kufikia uzalishaji wa samaki wa asilimia 50 kwa njia ya kufuga na asilimia 50 wanaotokana na maji ya asili.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji Dk Christine Ishengoma, aliipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka jitihada kuhakikisha inazalisha kwa wingi

vifaranga vya samaki na kutoa elimu juu ya ufugaji wa samaki.

Dk Ishengoma alisema kamati hiyo itaangalia vyema bajeti ya wizara itakayowasilishwa kwa ajili ya Mwaka wa Fedha 2021/22 ili iweze kuwa na tija na kuleta matokeo chanya hususan katika tasnia ya ufugaji samaki kwa kuwa bado ni eneo jipya ambalo watu wengi wanahitaji kujifunza na kujiingiza katika ufugaji huo.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ukuzaji Viumbe

Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Imani Kapinga, alisema Kituo cha Kingolwira kilichopo mkoani Morogoro, katika kutekeleza majukumu yake kati ya mwaka 2010 hadi 2020, kimetoa mafunzo kwa wananchi 11,280 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema licha ya kutoa mafunzo kwa wananchi, kimezalisha vifaranga vya samaki aina ya sato zaidi ya milioni sita vilivyosambazwa maeneo mbalimbali nchini.